



duducaello.com

AFYA YA UDONGO AU RUTUBA YA UDONGO NI NINI?

Afya ya udongo ni ule uwezo wa udongo kufanya kazi kama kitu chenye uhai ndani ya mfumo wa mazingira. *Mfumo wa mazingira* unamaanisha vitu vyote vyenye uhai kwenye mazingira yanayotuzunguka (viumbe hai vidogo sana, mimea, wanyama, binadamu) na mahusiano/maingiliano miongoni mwao na mazingira (hewa, tabia nchi, udongo, jua, hali ya hewa n.k.).

Udongo wenye afya huendeleza viumbe hai vinavyoishi ndani yake na kukuza afya ya mimea na wanyama walio juu yake, na kuendeleza na kuongeza ubora wa maji katika mito yetu na hewa inayotuzunguka.

Kupanda aina mbalimbali za mimea ambayo ni mwafaka/sahihi kwa udongo na tabia nchi ni muhimu sana kwa afya ya udongo. Mimea tofauti hutoa aina tofauti za vyakula kwa viumbe hai tofauti kwenye udongo. Matokeo yake, viumbe hai hivyo huipatia mimea maji na virutubisho muhimu.

Udongo wenye afya hupunguza hitajio la pembejeo za nje (mbolea na viutilifu) na hii inamaanisha ongezeko la faida kwa wakulima.